

Darasa la I

MAFUNZO YA BIBLIA KWA WATOTO

Kuifungua Biblia

by Denis & Devis Julius



MADARASA YA WATOTO: Sunday School.

DARASA LA KWANZA: BIBLIA

~Nuru ya upendo.

UTANGULIZI:

Kama mzazi/mlezi/ mwalimu, unawajibu kwa kumfundisha mtoto kwanza 'kuifungua biblia yake'. Kabla ya kuelezwa mafundisho yaliyo ndani yake. Hivyo utangulizi huu, akifundishwa vema utamwekea msingi mzuri wa kuitambua biblia, hata baadaye atakapoanza kujisomea mwenyewe.

Kumbuka wakati huu wa utoto, uwezo wake wa 'kukariri' ni mpana tofauti na wako, hivyo tumia fursa hiyo mapema kumjazia BIBLIA ndani yake. Mweke kwenye darasa kabisa maalumu wewe kama mzazi, walau mara mbili kwa wiki, saa mbili mbili, au jumapili katika madarasa yao ya watoto kanisani ikiwa wewe ni mwalimu wa watoto.

Mafundisho haya ni maalumu kwa watoto wenye umri wa miaka 0-12. Mwongozo huu utumie wewe kumfundisha. Lakini ikiwa upo Daresalaam /Arusha/Geita na utapenda pia mwanao afundishwe biblia kila jumamosi/jumapili na wenzake basi, wasiliana nasi kwa namba hizi. bure +255693036618/ +255789001312.

Mithali 22:6 Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.

BIBLIA.

Mwl: Biblia ni nini?

Watoto: *Ni kitabu kinachoeleza habari ya ukombozi wa mwanadamu ulioletwa na YESU KRISTO, BWANA WETU.*

Mwl: Biblia ina vitabu vingapi?

Watoto: *sitini na sita (66)*

Mwl: Biblia imegawanyika katika sehemu kuu ngapi?

Watoto: *Mbili (2)*

Mwl: Zitaje

Watoto: *Agano la Kale na Agano jipya*

Mwl: Agano la kale lina vitabu vingapi?

Watoto: *Thelathini na tisa (39)*

Mwl: Agano jipya lina vitabu vingapi?

Watoto: *Ishirini na saba (27)*

Mwl: Vitaje vyote.

Watoto: *(Wanavitaja, bila kusoma, au kukumbushwa)*

Akishafuzu darasa hili, ndipo apewe nafasi ya kuendelea darasa linalofuata. Waweza kutumia msaada wa nyimbo kumsaidia kukariri kwa haraka vitabu vyote vya biblia. Mpe mazoezi ya mara kwa mara, mpongeze kwa zawadi, afanyapo vizuri, lakini pia aonyeshapo kutozingatia/kiburi, tumia ukali kidogo, ikiwezekana fimbo agope arejee kwenye mstari, utamponya.

Mithali 22:15 Ujinga umefungwa ndani ya moyo wa mtoto; Lakini fimbo ya adhabu itaufukuzia mbali.

Ukizingatia vizuri kumfundisha, na kumpa mazoezi mara kwa mara ndani ya wiki mbili, atakuwa ameshakariri vitabu vyote.

MGAWANYO WA AGANO LA KALE:

(Mwonyeshe kwa mifano, ukifungua biblia kumwonyesha kimoja baada ya kingine kwenye mwongozo pale mwanzoni, baadaye ndio avijate mwenyewe kimigawanyo).

Mwl: Vitabu vya sheria ni vingapi?

Watoto: Vitano (5)

Mwl: Vitaje

Watoto: Mwanzo, Kutoka, Mambo ya walawi, Hesabu, Kumbukumbu la Torati.

Mwl: Vitabu vya historia agano la kale ni vingapi?

Watoto: Kumi na mbili (12)

Mwl: Vitaje

Watoto: Yoshua, Waamuzi, Ruthu, 1Samweli, 2Samweli, 1Wafalme, 2Wafalme, 1Mambo ya Nyakati, 2Mambo ya Nyakati, Ezra, Nehemia, Esta.

Mwl: Vitabu vya Mashairi agano la kale vipo vingapi?

Watoto: Vitano (5)

Mwl: Vitaje

Watoto: *Ayubu, Zaburi, Mithali, Mhubiri, Wimbo ulio bora*

Mwl: Vitabu vya Manabii agano la kale vipo vingapi?

Watoto: *Kumi na saba (17)*

Mwl: Vitaje

Watoto: *Isaya, Yerima, Maombolezi, Ezeieli, Danieli, Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Sefania, Hagai, Zekaria, Malaki*

(Akifanikiwa kwa ufasaha kuvigawanya mwenyewe vitabu hivyo vya agano la kale, ndipo aendelee na darasa linalofuata. Mkazanie aweze kufanya hivyo ndani ya wiki 2)

MGAWANYO WA AGANO JIPYA:

(Mwonyeshe kwa mifano, ukifungua biblia kumwonyesha kimoja baada ya kingine kwenye mwongozo, baadaye ndio avijate mwenyewe kimigawanyo).

Mwl: Vitabu vya injili vipo vingapi?

Watoto: *Vinne (4)*

Mwl: Vitaje

Watoto: *Mathayo, Marko, Luka, Yohana*

Mwl: Vitabu vya historia vipo vingapi?

Watoto: *Kimoja (1)*

Mwl: Kitaje

Watoto: *Matendo ya mitume.*

Mwl: Nyaraka za mtume Paulo zipo ngapi?

Watoto: *Kumi na tatu (13)*

Mwl: Zitaje

Watoto: *Warumi, 1Wakorintho, 2Wakorintho, Wagalatia, Waefeso, Wafilipi, Wakolosai, 1Wathesalonike, 2Wathesalonike, 1Timotheo, 2Timotheo, Tito, Filemoni*

Mwl: Nyaraka kwa watu wote zipo ngapi?

Watoto: *Nane (8)*

Mwl: Zitaje

Watoto: *Waebrania, Yakobo, 1Petro, 2Petro, 1Yohana, 2Yohana, 3Yohana, Yuda*

Mwl: Nyaraka za kinabii agano jipya zipo ngapi?

Watoto: *Moja (1)*

Mwl: Zitaje:

Watoto: *Ufunuo wa Yohana.*

Akifanikiwa kumaliza darasa hili kwa wiki 2. Ukijumlisha na zile wiki 4 za kwanza, ni mwezi mmoja na nusu . Mtoto atakuwa ameweza kuifungua biblia yake, na kuigawanya. Hata Yule ambaye hajui kusoma iwapo imekaa kichwani mwake vema baadaye haitamsumbua pindi awezapo kusoma. Zingatia tu wewe kama mzazi kumfundisha.

Usikose darasa la pili..

*****MWISHO*****

Mawasiliano.

Huduma ya Nuru ya Upendo wa Kristo.

www.wingulamashahidi.org

+255789001312/ +255693036618

info@wingulamashahidi.org